# HALMASHAURI YA MJI KONDOA

## HABARI ZA WIKI

JUMATATU, JAN 23-29, 2023

### ELIMU MSINGI



## PROGRAMU YA SHULE BORA ITASAIDIA KUINUA KIWANGO CHA UFAULU DODOMA"- DKT. FATUMA

KATIBU tawala Mkoa wa Dodoma Dk.Fatuma Mganga amesema kuwa moja ya matamanio yaliyopo kwa sasa mkoani hapo kwa mwaka 2023 ni kuongeza ufaulu kwa asili 95 ya matokeo ya mtihani wa darasa la saba na angalau asilimia 75 ya wanafunzi wanaohitimu kidato Cha Nne Wawe na ufaulu wa daraja la 1-3.

Dkt.Mganga ameyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya program ya Serikali ya SHULE BORA kwa waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma yaliyofanyika Januari 27,2023 wilayani Kondoa.

Mradi wa Shule Bora ni Programu ya Serikali Tanzania,ikifadhiliwa na Serikali ya Uingereza kwa lengo la kuinua ubora wa elimu ya Awali na Msingi katika mikoa tisa (9) hapa nchini kwa ushauri elekezi kutoka Cambridge Education ikishirikiana na mashirika ya ADD International, International Rescue Committee na Plan International.

"Mradi huu wa Shule Bora unatupa nguvu na matumaini makubwa kama mkoa kuona kuwa tunaweza kufikia malengo yetu angalu kuongeza ufaulu kwa asili 95 ya matokeo ya mtihani wa darasa la saba na angalau asilimia 75 ya wanafunzi wanaohitimu kidato Cha Nne Wawe na ufaulu wa daraja la 1-3,"amesema Dk.Mganga

YALIYOMO NDANI


**KAMATI ZA UJENZI ZATAKIWA KUKAMILISHA UJENZI UK. 4**

**KT.MKANACHI AWATAKA WALIMU WA MSINGI KUVITUMIA VISHKWAMBI KUONGEZA UFAULU UK. 5**

**"TUMIENI KIINGEREZA MUWAPO SHULENI"- AFISA ELIMU SEKONDARI UK. 6**

**KAMATI YA SIASA KONDOA YAMPONGEZA MNUFAIKA WA MIKOPO YA ASILIMIA 10 UK.7**




INATOKA UK 1

## PROGRAMU YA SHULE BORA ITASAIDIA KUINUA KIWANGO CHA UFAULU DODOMA"- DKT. FATUMA

Dkt.Mganga amesema kuwa Mwaka huu peke yake zaidi ya wanafunzi elfu 90 wanatarajiwa kuanza masomo ambapo Mpaka kufikia Januari 26.2023 asilimia 89.7 ya wanafunzi wa darasa la awali walioripoti shule,huku asilimia 94.2 Kwa darasa la kwanza na asilimia 66.95 kidato Cha kwanza wakiwa wameripoti shule.

Naye Mratibu wa Program ya SHULE BORA Mkoa wa Dodoma Mtemi Zombwe amesema kuwa ili kufanikisha mchakato wa kuinua na kuboresha elimu ni vyema kila mmoja akatambua kuwa anajukumu la kushiriki katika mchakato huo.

"Mradi wa SHULE BORA ni Programu mahususi kabisa kwa ajili ya kuinua na kuboresha ubora wa elimu hivyo ili tufaniliwe ni lazima kila mmoja ajue ana wajibu wa kuhakikisha elimu inakuwa bora,"


Mradi unalenga kuwa na matokeo makubwa na endelevu katika elimu ,kwa kusaidia kuanzisha na kuimarisha mifumo na taratibu za elimu ,kwa kufanya hivyo ,mpango utaimarisha matokeo ya ujifunzaji,hususani katika KKK na kiwango cha wanafunzi kusailia shule,"amesema Zombwe

Mradi wa SHULE BORA utatekelezwa katika mikoa 9 ikiwemoDodoma,Mara,Katavi,Rukwa,Kigoma,Singida, Simiyu,Pwani na Tanga hadi ifikapo mwaka 2027 kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza kupitia mfuko wa UK aid kwa gharama ya poundi za Kiingereza milion 89 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 271.

Hata hivyo Katibu tawala huyo amesema kuwa swala la Elimu katika Mkoa wa Dodoma bado halijatangazwa vizuri na kuwataka waandishi wa habari wakawe chachu katika kuielimisha jamii kuwa wanajukumu la kushiriki kikamilifu katika kuboresha elimu.

"Naamini mara baada ya kumalizika kwa mafunzo haya mtakwenda kuifungua jamii kifikra kuwa wana jukumu la kushiriki katika kuinua ubora wa elimu katika Mkoa wetu na naomba sana kwenu waandishi mwaka huu Dodoma tumebeba agenda yetu ya sekta ya elimu hivyo kupitia nyinyi tunaamini itafanikiwa kwani nyinyi mkiamua kutumia vyombo vyenu hakuna kitakachoshindikana,"ameongeza Dkt.Mganga

Ambapo Dkt.Mganga ameeleza kuwa kwa sasa mkoa wa Dodoma una upungufu wa vyumba vya Madarasa zaidi ya 7000 ndipo akapeleka ombi kwa wazazi na jamii kwa ujumla kujikita katika kuhakikisha kila mwaka katika gitongoji,kata na mitaa yao wanaweza kujenga angalau chumba kimoja cha darasa ili kuwasaidia watoto wenye umri wa kwenda shule kuanza masomo.



## ZIARA KAMATI YA FEDHA



# KAMATI ZA UJENZI ZATAKIWA KUKAMILISHA UJENZI

Kamati zinazosimamia miradi ya ujenzi wa zahanati mtaa wa Ausia na Mulua wametakiwa kuongeza nguvu katika usimamizi wa ujenzi wa zahanati hizo ili zikamilike na kutoa huduma kwa wananchi.

Hayo yamesemwa na wajumbe wa kamati ya Fedha na Utawala wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi iliyofanyika hivi karibuni.

"Simamieni vituo vianze kufanyakazi wananchi wapate huduma tunapochelewa tunajichelewesha wenyewe na kuwatesa wananchi wanaotembea umbali mrefu kupata huduma,"amesema Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Mhe. Mohamed Kiberenge

Ameongeza Mhe.Kiberenge kwa kuwaeleza wanakamati hao kiwa zahanati hizo lazima zikamilike na Halmashauri italeta fedha za ukamilishaji kadiri wanavyokusanya mapato na kipaumbele kitakuwa kwa zahanati hizo.

Aidha wajumbe hao wametoa angalizo kwa kamati hizo kutofanya malipo kwa mafundi nje ya mkataba kwani kwa kufanya hivyo ni kinyume na taratibu ambazo zinamtaka fundi kujenga kwanza ndipo malipo yafuate.

Hata hivyo wameipongeza kamati ya mradi wa Mlua kwa hatua waliyofikia na kuwataka kumsimamia fundi anayeendelea na kazi kumaliza kazi iliyobakia ndani ya wiki moja.

Ziara ya Kamati ya fedha na Utawala imefanyika ikiwa ni ajili ya kukagua miradi kwa robo ya pili ambapo imepitia miradi ya ujenzi wa zahanati ya Ausia, Mlua ambao walipewa shilingi milioni 50 kila zahanati na zipo hatua za ukamilishaji ikiwa ni pamoja na kutembelea miradi ya ujenzi wa kituo vha Afya Kolo na ukarabati shule ya Msingi Kolowasi.





## UGAWAJI WA VISHKWAMBI



## DKT.MKANACHI AWATAKA WALIMU WA MSINGI KUVITUMIA VISHKWAMBI KUONGEZA UFAULU

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Mhe. Dkt. Hamisi Mkanachi amewataka walimu wa Shule za Msingi kwenda kuvitumia vishkwambi walivyopewa katika kuongeza ufaulu kutoka nafasi ya 3 kimkoa na kuwa wa kwanza kimkoa na 10 bora kitaifa.

Ameyasema hayo wakati wa hafla fupi ya kukabidhi vishkwambi 257 kwa walimu wa Shule za Msingi za Halmashauri ya Mji Kondoa iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

“vishkwambi hivi vikaongeze asilimia ya ufaulu kwa wanafunzi kwa kuwa kila mwalimu anapewa cha kwake na tusikubali tufanye mabadiliko kwa kuionyesha Kondoa kama Kondoa na inawezekana,”amesema Dkt. Mkanachi

Aidha ameongeza kuwa pamoja na yote vishkwambi hivyo vikazibe upungufu wa walimu uliopo kwani itawaongezea uwezo wa kujiongezea maarifa kwa kuwa hiyo ni teknolojia na pia vitaongeza kuongeza hali ya wanafunzi kupenda shule na kupunguza utoro.

Ameongeza kwa kuwataka walimu kwenda kuvitumia vizuri vishkwambi hivyo kama ilivyokusudiwa ili vikalete tija kwa taifa hivyo wanapaswa pia kuvitunza.

Halmashauri ya Mji Kondoa imepokea vishkwambi 257 kutoka Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya walimu wa shule za msingi ambapo imefanyika hafla ya kuwapa walimu wote wa Shule za Msingi na mgeni rasmi alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Kondoa.





## ELIMU SEKONDARI



## "TUMIENI KIINGEREZA MUWAPO SHULENI"- AFISA ELIMU SEKONDARI

Wanafunzi wa kidato cha kwanza Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kutumia lugha ya kiingereza wawapo shuleni kwa kuwa ndio lugha ya mawasiliano katika shule za Sekondari.

Kauli hiyo imetolewa na Afisa Elimu Sekondari Mwalimu Annette Nara alipokuwa akiongea na wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Gubali ikiwa ni ziara yake ya ufuatiliaji wanafunzi wa kidato cha kwanza.

"Hakuna atakayekucheka ukikosea sababu wote hapa tunajifunza na mmekuwa mkifundishwa kiingereza toka mlipokuwa darasa la tatu hivyo fanyeni mazoezi tu ya kuongea kiingereza mtaweza,"amesema Mwalimu Nara

Ameongeza kwa kusema kuwa lugha ya kiingereza inafanyiwa mazoezi hivyo kwa kukaa kimya haitawasaidia sababu watakuwa hawajifunzi na hiyo ndio lugha ya masomo yote isipokuwa somk la kiswahili.

"Rafiki zenu ambao wamefaulu na hajaripoti shuleni kawaambieni waje shuleni kwani serikali itakuja kuwakamata pamoja na wazazi na walezi wao na kuwafunga gerezani mnataka kufungwa mpoteze ndogo zenu?"ameuliza Mwalimu Nara

Aidha amewapa moyo kwa kuwaambia wote wana akili na hakuna mjinga kati yao kwani kufaulu ni juhudi za mwanafunzi kwa kuzingatia nidhamu, kutii kanuni za shule na kuhudhuria vipindi vyote.

Hata hivyo Afisa Elimu alimpa motisha ya fedha Mwalimu Mzava wa somo la kiswahili kutoka a na wanafunzi kufaulu somo hilo katika mtihani wa taifa wa kidato cha pili na kuwasihi walimu wengine kuongeza bidii katika ufundishaji ikiwa ni pamoja na kuzingatia maagizo yote waliyopewa wakati wa kikao cha elimu ngazi ya mkoa.





## ZIARA KAMATI YA SIASA(W)



# KAMATI YA SIASA KONDOA YAMPONGEZA MNUFAIKA WA MIKOPO YA ASILIMIA 10

Kamati ya siasa Wilaya ya Kondoa imempongeza kijana Hashimu Juma mwenye ulemavu kwa kutumia vizuri na kurejesha mkopo aliopewa na Halmashauri ya Mji Kondoa.

Pongezi hizo wamezitoa wakati wa ziara ya kamati hiyo kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri ya Mji.

Akiongea Katibu wa CCM Wilaya ya Kondoa Ndg. Ibrahim Mpwapwa amesema amempongeza kwa kumaliza mkopo kwa kuwa wengine wasio na ulemavu wanasumbua kufanya marejesho.

Aidha ameongeza kuwa ombi lake la kuongezwa fedha limezingatiwa na litafanyiwa kazi kwa jinsi halmashauri inavyopata mapato.

Akiongea Ndg.Hashim Juma amemshukuru Rais Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fursa ya mikopo inayosaidia vijana kupata kipato na kuendesha maisha yao.

Aidha ameiomba Halmashauri kumuwezesha awamu ya pili mkopo shilingi milioni 20 ili aweze kununua gari litakalomuwezesha kununua malighafi na kusambaza unga anaozalisha mwenyewe pia amewashauri vijana kutumia fursa za mikopo inayotolewa na vijana.

Hashimu aliwezeshwa fedha shilingi milioni 3 kutoka Halmashauri ya Mji kutokana na mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ambapo amenunua mota ya mashine ya kusaga na anazalisha unga na kusaga kwa wanajamii na anatarajia kumaliza mkopo mwezi februari 2023.






# TAARIFA MBALIMBALI/MATANGAZO YA IDARA

## UHUISHAJI WA LESENI ZA BIASHARA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWAKUMBUSHA WAFANYABIASHARA WOTE WA KONDOA MJI KUHUISHA LESENI ZA BIASHARA KWA ZILIZOKWISHA MUDA NA ZINAZOKARIBIA KUMALIZA MUDA WA MATUMIZI.

AIDHA WOTE AMBAO WATAKUTWA BILA LESENI AU ZIMEKWISHA MUDA WATALIPA ASILIMIA 20 YA BEI YA LESENI YA BIASHARA WANAYOFANYA.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

## ULIPIAJI WA KODI YA VIBANDA VYA HALMASHAURI

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWAKUMBUSHA WAPANGAJI WOTE WA VIBANDA VYA HALMASHAURIVILIVYOPO KATIKA SOKO KUU NA STENDI YA MABAS KULIPA KODI YA PANGO KABLA AU IFIKAPO YA TAREHE 5/02/2023.

WALE WOTE AMBAO HAWATAKUWA WAMELIPA KODI WATALAZIMIKA KULIPA FAINI AMBAYO NI ASILIMIA 20YA BEI YA PANGO.

HIVYO ILI KUEPUKA KULIPA FAINI HIYO UNAKUMBUSHA KUFIKA KATIKA OFISI ZA UHASIBU KATIKA JENGO LA ZAMANI LA HALMASHAURI KARIBU NA MAHAKAMA YA WILAYA KWA AJILI YA KUCHUKUA NAMBA YA MALIPO (CONTROL NUMBER) NA KULIPIA.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

## ULIPIAJI WA TOZO ZA TAKA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA KONDOA MJI KULIPA TOZO KWA AJILI YA HUDUMA YA UBEBAJI WA TAKA KATIKA MITAA YAO.

AIDHA ANAWATAKA KUFANYA USAFI KWA KUZIBUA MITARO ILI MAJI YA MVUA YAKIJA YAPATE SEHEMU ZA KUPITA IKIWA NI PAMOJA NA KUPIGA MARUFUKU WANANCHI KUTUPA TAKA KATIKA MITARO.

PIA WANANCHI MNATAKIWA KUFANYA USAFI KATIKA MAENEO YANAYOWAZUNGUKA NA MAPAGARE KWA KUFYEKA NYASI.

WATAKAOKUTWA WANATUPA TAKA MITARONI NA AMBAO HAWAJAZIBUA MITARO FAINI NI SHILINGI ELFU HAMSINI.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

# MIRADI MBALIMBALI ILIYOTEMBELEWA KATIKA WIKI




KITUO CHA AFYA KOLO




UJENZI WA MADARASA KATIKA SHULE YA MSINGI KOLOWASI



MADARASA YA UKARABATI KATIKA SHULE YA MSINGI KOLOWASI



UCHIMBAJI WA MISINGI KATIKA HOSPITALI YA MJI KONDOA KWA AJILI YA KUJENGA JENGO LA MAMA NA MTOTO,MOCHWARI NA JENGO LA UPASUAJI.




JENGO LA CHOO KWA NJE NA NDANI KATIKA STENDI YA MABASI BICHA